# "ULEMAVU BARANI AFRIKA"
# EPISODE 2: "NISAMEHE…"

**AUTHOR: Chrispin  Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 2:**

**MSIMULIZI**

**SCENE ONE: EVENING AT FAGILIO'S HOUSE**

- Fagilio (mume, 42)
- Tofa (mke, 40)
- Chitoto (mume,19)

**SCENE TWO : EVENING BY THE BAOBAB TREE**

- Oluanda (mume, 18)
- Porojo (mume, 60)
- Tofa (mke, 40)
- Karemi (mume, 18)

**SCENE THREE : EMERGENCY UNIT AT THE HOSPITAL**

- Dkt. Esther (mke, 45)
- Tofa (mke, 40)

**SCENE FOUR : IN OLUANDA'S CLASSROOM**

- bi. Nina (Mke, 45)
- darasa la mseto (wake/waume, 18+)
- Kangwa (mume, 18)
- Chitoto (mume, 19)
- Karemi (mume, 18)

## SCENE FIVE : RECOVERY HOSPITAL WARD

- Oluanda (mume, 18)
- Tofa (mke, 40)

### UTANGULIZI:

Nawasalimu tena na tena katika makala mapya yakujifunza redioni, **Noa bongo, jenga maisha yako**. Tuko kwenye kipindi cha pili cha tamthilia kwa isimu “ **Ulemavu barani Afrika**”. Kipindi kilichotupa kisogo, Oluanda alianguka na kujivunja mguu na kukanyagwa na gari lililokwenda kasi. Hii ilikuwa jaza yake baada ya kumdanganya mamake, Tofu kwamba anakwenda kuchukua kitabu cha historia kwa kina Chitoto. Pia tukamshuhudia Karemi na dadake Zabibu, ambaye ni zeruzeru, waliishi na nyanya yaoTheresa. Tuliiacha hadithi yetu nyumbani kwa Fagilio ambapo Tofu amesimama mbele ya Chitoto na babake, akitaka kujua alipokuwa mwanae, Oluanda.
Sasa tamakani, tulia, sikiliza na ujifunze katika kipindi hiki kilicho orodhesha neno moja muhimu..“ **Nisamehe** ”

**SCENE ONE : EVENING AT FAGILIO'S HOUSE**

1. **SFX: EVENING AMBIENCE / MOSQUITOES, CRICKETS etc.**

2. **TOFA:** (**agitated)** Chitoto!Utanieleza pale mwanangu !aliko au utakaa kimya ukinitumbulia macho kama kichakulo?

3. **FAGILIO:** Tofa! Tosha! Mwanangu hajui pale mwanao Oluanda aliko. Kama ni mimi nisingelijitia taharuki kutafuta kijana na akili zake. Ni mtu mzima yule, hata labda anastarehe na kasichana huko nje.

4. **TOFA:** **(cuts Fagilio short**) Niambieni aliko basi! Na kwa taarifa yako, Fagilio kuna tofauti kubwa kati ya Oluanda na Chitoto, Oluanda hajawahi kunidanganya. Chitoto, anza kuzungumza.

5. **CHITOTO:** **(Scared voice)** Sii.... Sii.. Sijui kule Oluanda aliko. Tulionana mwisho tulipotoka shuleni. Labda yuko na kina Karemi na Magoto. Niliskia wakisema watakwenda kuangalia mashindano ya magari ya safari rali…

6. **FAGILIO:** Natumai umeridhika! Sasa tafadhali ondoka nyumbani kwangu. Na ukijaaliwa kuja tena kwangu… niletee kanywaji…kwaheri.

7. **SFX : WOODEN DOOR WITH HINGES CLOSED**

8. **TOFA:** **(Nervously talking to herself)** Kwa hivyo, Oluanda anataka kunifanya mimi mjinga. sawa, tutaona nani mahiri. Najua pale Karemi na dadake wanaishi. Oluanda hajui kinachomsubiri….

9. **SFX : HURRIED FOOTSTEPS ON DUSTY RUGGED PATH**

10. **MSIMULIZI:** Akiwa na hamaki, wasiwasi na hofu, Tofa aliondoka nyumbani kwa Fagilio na kuelekea kwa kina Karemi. Wasiwasi mkuu ulimjia, lakini hakujua yatakayomsibu..Pale mbuyuni,Oluanda bado hakuwa na fahamu hadi Porojo, muuguzi wa kienyeji, alipokuwa anachuna dawa za miti shamba na kuziweka kwenye Mkokoteni wake, kwa bahati akamuona…

**<u>SCENE TWO: EVENING BY THE BAOBAB TREE</u>**

11. **SFX: OUTSIDE AMBIENCE, BIRDS; CRICKETS; WIND IN THE TREES; WHEELBARROW BEING PUSHED**

12. **POROJO:** (**Surprised)** Mungu wangu! Ni nini hii? Kijana, enuka! Uko mzima kweli? Amka kijana!

13. **SFX : GENTLE TAP ON FACE SEVERAL TIMES**

14. **OLUANDA:** **(In agony)** Arrrgh!... Niko wapi? Ah mguu wangu, siwezi kuuinua... unaniuma vibaya sana.

15. **POROJO:** Kweli, mguu wako wa kushoto umeumizwa sana, mifupa yake imevunjwavunjwa kabisa. Umeumia saa ngapi? Unaweza kukumbuka kulitokea kitu?

16. **OLUANDA:** **(In agony)** Tafadhali nisaidie, nipeleke kwa mamangu.nisaidie.. naumwa!

17. **POROJO:** Usijali, mimi ni mtabibu naitwa Porojo. Mguu wako umeumia sana, kwanza nitajaribu kuagua,Nitaufunga kwa kutumia vijiti na kitambaa ili ushikamane kidogo. Kwa sasa shuka yangu itafaa.

18. **SFX: BREAKING OF STICKS AND TEARING OF OLD MATERIAL**

19. **POROJO:** Utasikia maumivu kwa hiyo jikaze kiume.

20. **MSIMULIZI:** Wakati Porojo akipeana huduma ya kwanza, ambayo ilikua ishachelewa kuuafu mguu wa Oluando, Tofa, mamake Oluanda, na Karemi walifika mbuyuni, wakiwa na kibatari mkononi, Tofa alikuwa wa kwanza kumuona mwanaye akipewa huduma ya kwanza….

21. **TOFA:** **(Shouts)** Wewe! Hebu muache mwanangu! Unamfanya nini... Mungu wangu! Oluanda umefanyika nini? **(tearful voice)**

22. **OLUANDA:** Mama, mama, nisamehe. Tafadhali nisamehe.

Nisamehe.

23. **POROJO:** Mama, mtoto wako ameumia sana, Nilimpata hapa amelala na amepoteza fahamu na ni muhimu umkimbize hospitali. Siwezi kumsaidia zaidi ya hapo.

24. **TOFA:** Shukurani sana. Mwanangu Oluanda, utapata nafuu. Jipe moyo. Sasa tutafika vipi hospitali bila ya usafiri, huo mguu unaonekana hauwezi kutembea….

25. **POROJO:** Tumieni mkokoteni wangu. Dawa zangu hazina neno hata nikizichukuwa kesho. Ukitaka naweza kuandamana nanyi hadi hospitali….

26. **TOFA:** La, asante sana. Umetusaidia vyakutosha, Porojo. Karemi tafadhali tumuenue Oluanda tumueke kwenye mkokoteni.

27. **POROJO:** Kuweni waangalifu musiutingishe mguu. Acha niwasaidie.

**(They act out lifting Oluanda)**

**28. SFX: Boys body being lifted**

29. **POROJO:** Chumba cha wagonjwa mahututi huwa wazi masaa 24 kwa hivyo lazima watakuwa tayari kuwasaidia. Koma za mababu zetu na waganguzi ziwe nanyi.

30. **KAREMI:** Oluanda pole sana, mamake Oluanda nitakuelezea kila kitu tukiwa njiani. Tuharakishe tuondoke sasa.

31. **TOFA:** Ndio, maadamu nina kibatari basi nitakuongoza njia. Na Karemi usinifiche kitu.

32. **SFX :** **WHEELBARROW BEING PUSHED**

33. **MSIMULIZI:** Walienda kwa uangalifu na Oluanda, huku Karemi akimhadithia Tofa kila kitu na hata walivyoekeana ahadi kuhusu mashindano hayo ya magari. Hatimaye, waliwasili hospitali na walipofika pale, Oluanda alichukuliwa kwa picha ya x-ray. Baada ya muda, daktari Esther, ambaye alikuwa zamu usiku huo alikuja na majibu ya picha hiyo….

**SCENE THREE: EMERGENCY UNIT AT THE HOSPITAL**

**34. SFX: : HOSPITAL AMBIENCE**

35. **DKT. ESTHER:** Mimi ni Daktari Esther...na..

36. **TOFA:** Mwanangu anaendeleaje? Hali yake ikoje?

37. **DKT. ESTHER:** Ehhm....Nasikitika, Hairidhishi. Mguu wake uliumia vibaya sana na mifupa imepondeka kabisa. Aliniambia ni gari lilimgonga na kutoroka. Inaonekana hatoweza kuutumia tena mguu wake…

38. **TOFA:** Ati ? Unamaanisha nini daktari?

39. **DKT. ESTHER:** Ni lazima uwe mkakamavu sasa na umsaidie kijana wako , ni lazima tuukate mguu wake, picha ya x-ray imetuonyesha hatuna budi ila kuukata.

40. **TOFA:** Muukate? Yani muukate mguu wake kabisa? La! Haiwezekani! Mguu wake anauhitaji. Wewe akili yako ni timamu? Unawezaje kufikiria kitu kama hicho?

41. **DKT.ESTHER:** Mama suluhisho ni hilo pekee. Hatuna jengine. Ni lazima tuukate na nahitaji ruhusa yako ili tuendelee.

42. **TOFA:** Ninaweza angalau kuzungumza na yeye? **(in tears)**

43. **DKT.ESTHER:** Tumempatia dawa za kulala,kwa hiyo hawezi kuzungumza. Najua huu ni uamuzi mgumu kuchukua. Lakini ni kwa usalama wake.

44. **TOFA:** Sasa baadaye kutakua vipi? Atakapoamka na kupata hana tena mguu wa kushoto? Nitamueleza vipi? Kijana wangu atakua kilema. Mola wangu, mbona haya yatupate sisi?

45. **DKT.ESTHER:** Kijana wako atakumbwa na changamoto, ya jinsi ya kutembea tena. Lakini hakuna sababu ya yeye kutoishi maisha ya kawaida

51. kama awali. Bado nasubiri kauli yako. ukikubali, tafadhali weka sahihi katika nakala hizo na umpe nesi wa zamu. Nataka kumuona na kuwaona wagonjwa wengine.

46. **SFX:** **SHUFFLING OF PAPERS AND PEN SCRIBBLING**

47. **TOFA:** Daktari subiri kidogo, (**pause)** sawa tafadhali endelea. Mungu wangu, nisamehe.

48. **DKT.ESTHER:** Usihukumike,uamuzi wako ni kwa manufaa yake kwa sasa. Atakuelewa.

49. **MSIMULIZI:** Na anapoweka sahihi ishara ya kukubali, Tofu alikuwa amewaruhusu madaktari waukate mguu wa mwanae Oluanda uliokuwa umevunjika pasi matibabu. Oparesheni ilikua ngumu lakini baada ya muda mfupi Oluanda alikuwa ameshapelekwa chumba cha manafuu huku mamake akimkagua na machozi tele machoni. Asubui iliyofuatia darasani kwa kina Oluanda, Bi. Nina mwalimu wa Oluanda, alikuwa tayari kuanzisha somo la kwanza.

**<u>SCENE FOUR: AT  OLUANDA'S CLASSROOM</u>**

50. **SFX:** **NOISY CLASSROOM DISCUSSING ABOUT OLUANDA'S ACCIDENT**

51. **BI. NINA:** Habari zenu!

52. **CLASS:** Nzuri mwalimu Bi. Nina.

53. **BI. NINA:** Oluanda yuko wapi? Sio kawaida yake kuadimika shuleni. Chitoto, wewe, Karemi na Magoto nyinyi ni marafiki zake munajua ana nini?

54. **KAREMI:** Mwalimu, Oluanda yuko hospitali. Alipata ajali mbaya sana jana baada ya kuanguka kutoka juu ya mbuyu. Mimi na mamake ndiyo tulimpeleka hospitali.

55. **BI.NINA:** Inasikitisha mno. Lakini ni funzo kwenu nyote. Nyinyi munashindana na tumbili? Wale walizaliwa mitini. Nyinyi je?

56. **KANGWA:** Kwa kweli, mwalimu yale tuliyosikia ni kuwa chitoto hapa…

57. **CHITOTO:** Nyamaza Kangwa! Wajua nini ?

58. **BI. NINA:** Eh,kimya! Chitoto, neon moja zaidi na nitakutupa nje ya darasa! Tumuombeeni Mungu Oluanda apone haraka na arudi shule. Sasa fungueni ukurasa... **(voice fades out)**

59. **MSIMULIZI:** Habari kuhusu ajali ya Oluanda zilienea kama biwi la moto wakati wa kiangazi katika eneo la Maganye lakini hawakujua kuwa Oluanda alikuwa kitandani akiamkia mshangao

mshangao mkuu ambao hakuupangia wala kuutarajia.

**<u>SCENE FIVE: RECOVERY HOSPITAL WARD</u>**

**60. SFX: HOSPITAL AMBIENCE**

61. **OLUANDA:** **(Sleepy voice)** Mmmh

62. **TOFA:** Ssssh, Oluanda… Mwanangu... Nisamehe.. Nisamehe sikuwa na budi...

63. **OLUANDA:** Mama.. ni nini...la.. maumivu…! **(painfully)** Tafadhali... la….!

64. **TOFA:** Hawakuwa na budi… mwanangu, lisilo budi hutendwa. Najuwa ni uchungu, lakini iliwalazimu waukate mguu wako. Ulikuwa umejeruhiwa vibaya mno baada ya ajali. Mbona ukanificha? Lakini usihofu, naahidi sitokuacha kamwe.

**<u>HITIMISHO:</u>**

Huku husio hilo likibubujika kutoka kinywani mwa mama aliyepoteza tumaini.. aliyeketi ubavuni mwa mwanae aliye na jeraha bichi la kukatwa mguu, tunatatisha kipindi chetu cha redio kwa jina la “ **Ulemavu barani Afrika** ”. Ni yapi yatamsibu Oluanda atakapoanza Maisha mapya na changamoto ya matembezi? Marafiki, shule na jamii itamchukulia vipi katika hali hii ngeni? Kwa majibu ya maswali haya na zaidi jiunge nasi juma lijalo. Na unuiapo kutupa maoni, hoja au masaibu yaliyokukumba binafsi kuhusu maisha na changamoto za walemavu, tafadhali tembelea

tovuti zetu www.dw world.de/lbe. Tungelipenda kusikia kutoka kwako. Mpaka tutakapolitandika tena jamvi letu, kwaherini na kila la heri.